# TARGETER WINGS
# JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT
# GREDI YA SABA - 2024

Wings 004

# KISWAHILI

**Muda: Saa 1 dakika 20**

***Maagizo:***

***(a) Andika jina lako, la shule, nambari ya usajili na tarehe kwenye vihasho uliopewa.***

***(b) Jibu maswali yote kwenye karatasi hili.***

**Jina** ________________________________________________

**Shule** ________________________________________________

**Nambari ya Usajili:** ____________________ **Tarehe** ____________________

| MTAHINI PEKEE | | | |
|---|---|---|---|
| **Swali** | **Upeo wa alama** | **Alama ya mwanafunzi** | **Kiwango cha utendaji** |
| **1 - 29** | **Alama 50** | | |
| **Jumla** | **50** | | |

**1. UFAHAMU WA KUSOMA**

**I *Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 1 hadi 4***

Simba aliamuru wanyama wote kufika mkutanoni. Alikuwa amekerwa na tabia zao za ubinafsi na kutothamini udugu. Yamkini wanyama hawakuelewa kuwa udugu ni kufaana bali si kufanana. Kutokana na uchungu aliokuwa nao moyoni, alikata shauri ili waishi kwa utangamano.

"Ndugu wenzangu, katika dunia hii kila mmoja yu mbioni kutafuta mali ili kuboresha maisha. Ukiwa na pesa nyingi, utaweza kuwa na makazi mazuri, chakula na mavazi bora. Ukiugua bila shaka utapata matibabu bora na hivyo kuwa na tumaini la kuishi miaka mingi duniani.

Hata hivyo, kuna baadhi ya vitu ambavyo huwezi kuvipata kwa kuwa una mali mengi. Hekima na afya bora ni majaliwa kutoka kwa Mungu. Hospitali za kifahari zimejaa matajiri ambao kando na uchungu wa kuugua, wanahofia kufa na kuacha mali yao.

Wanyama wenzangu, utajiri uletao furaha ni ule ambao umepatikana kwa kutoa jasho. Ukiwa mwenye bidii, utakuwa umetulia na kufurahia kula mali yako. Usiku utalala usingizi wa pono bila ndoto za kutisha. Kwa upande mwingine, utajiri uliotafutwa kwa njia za hila hauleti furaha maishani. Shida humwandama mwenye utajiri wa hila mchana kutwa na usiku kucha. Huogopa labda aliowatapeli mali yao huenda wakapanga njama ya kumwangamiza. Kwa hivyo ndugu zangu, tuishi bila ubinafsi na kuyathamini maisha ya wenzetu. Asanteni kwa kunisikiliza." Simba alikamilisha ushauri wake.

Wanyama wote walimpigia makofi mfalme wao na kuahidi kuishi kwa amani, umoja na upendo. Ngiri alipata afueni kwani alikuwa mmoja kati ya wanyama waliotapeliwa na Fisi.



CamScanner

1. Kwa nini Simba aliamuru wanyama wote kufika mkutanoni? ______
2. Hadithi hii imeonyesha kuwa kila mnyama alikuwa mbioni kujitafutia utajiri. Andika jambo moja lililowasukuma wanyama kutafuta mali. ______
3. Utajiri si kigezo cha kuwa na maisha bora duniani. Andika kauli moja kutoka kwenye kifungu kuthibitisha kauli hii. ______
4. Ni funzo gani upatalo kutokana na utajiri ulioletwa kwa njia za hila na ule apatao mtu kwa njia halali? ______

**II. *Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 5 hadi la 8.***

Teknolojia imechangia kuleta mfumo mpya wa maisha kote ulimwenguni. Matumizi ya tarakilishi yameenea kote na si mapya tena. Yameleta msukumo mpya wa maendeleo katika nyanja mbalimbali za nchi kama vile biashara, uvumbuzi wa bidhaa mpya viwandani na vyombo vya kuonewa fahari katika makazi ya watu vikiwemo runinga, majiko, redio na kamera za siri.

Dunia nzima imekuwa kama kijiji tu. Mawasiliano kati ya watu walio katika janibu za ughaibuni ni kana kwamba yanafanyika katika chumba kimoja. Mapatano na uhusiano wa watu huwa wazi zaidi. Hapo zamani, ilichukua muda mrefu sana kutuma nyaraka zilizochukua siku kadhaa kufika; siku hizi huduma hii ya shirika la posta si kizuizi kikubwa kwa mawasiliano na umuhimu wake umeachiwa uwasilishaji wa vifurushi kutoka sehemu moja ya nchi hadi nyingine.

Matumizi ya rununu kupitia arafa na matumizi ya baruapepe yameboresha mawasiliano. Ujumbe hufika upesi na gharama yake ni nafuu. Licha ya ufanisi huo wa mawasiliano kupitia teknolojia, pamezuka utata hasa mmomonyoko wa maadili. Licha ya mazuri yaletwayo na teknolojia, mengine hayana manufaa kwetu. Kuigaiga mila za kigeni kuna athari kwa tamaduni zetu.

5. Matumizi ya teknolojia yameleta maendeleo katika nyanja za biashara, uvumbuzi wa bidhaa viwandani, runinga, majiko, redio na kamera za siri. Mbali na biashara na uvumbuzi, taja sekta nyingine inayotumia teknolojia. ______
6. Mojawapo ya madhara ya teknolojia ni:
   A. kueneza habari za ulimwengu
   B. uigaji wa tamaduni za kigeni.
   C. kuelimisha idadi kubwa ya watu.
   D. kuunganisha ulimwengu na kuufanya kama kijiji kimoja.
7. Shirika la posta ni muhimu hasa katika shughuli ya
   A. kutuma na kupokea barua.
   B. matangazo ya bidhaa.
   C. usambazaji wa vifurushi.
   D. kutuma ujumbe kwa gharama ya chini.
8. Kisawe cha neno **'ughaibuni'** kama lilivyotumiwa kwenye kifungu ni:
   A. nchi za mbali
   B. nchi zenye ustawi
   C. nchi za karibu
   D. nchi za ulaya

## 2. UFUPISHO

***Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 9 hadi 12.***

Makazi machafu huwa na athari belele kwa wakazi. Magonjwa kama vile kipindupindu, homa iletwayo na mbu na hata homa ya matumbo hupenda makazi yasiyokuwa safi. Watu wanaoishi katika makazi machafu wanaelewa kuwa maisha ni kuisha. Magonjwa anuwai huathiri wakazi wanaoishi maeneo machafu.

Mbali na kuishi katika makazi safi, kuna mambo matatu muhimu ambayo huchangia afya ya mwanadamu. Kwanza, usafi wa kibinafsi. Aina hii ya usafi humpa mtu utulivu na kumwepusha na magonjwa ambayo yanaandama uchafu wa mwili.

Pili, usafi wa mawazo na akili ni muhimu katika afya ya mwanadamu. Usafi wa akili humshurutisha mtu kuwa mwadilifu. Daima atashiriki mambo ya kistaarabu na uungwana wake hudhihirika. Mwanadamu huwa na imani aitumiayo kama dira ya kumwelekeza maishani. Usafi wa kiroho humfanya mtu kuwa na msingi madhubuti wa imani. Tunapaswa kujaribu kadiri ya uwezo wetu kudumisha usafi wa sehemu za umma na kwa jumla mazingira yetu ili kujihakikishia hali nzuri ya afya.

9. Je, kichwa gani kinachofaa kifungu hiki?
______
10. Andika habari kuu inayojitokeza katika aya ya kwanza.
______

11. Kauli; 'Kwanza, usafi wa kibinafsi. Aina hii ya usafi humpa mtu utulivu na kumwepusha na magonjwa ambayo yanaandama uchafu wa mwili," imetumiwa katika kifungu. Fupisha kauli hii kwa maneno yasiyozidi 13.

____________________________________________________

____________________________________________________

____________________________________________________

12. Eleza kwa sentensi moja, manufaa ya usafi wa mawazo na akili kwa mwanadamu.

____________________________________________________

## 3. SARUFI

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 13 hadi 17. Umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Siku chache __13__ tulitembelewa na daktari wa afya ya umma. Alipofika shuleni __14__ kwa furaha. Alieleza kuwa tukitaka __15__ maradhi sharti tuzingatie usafi wa sehemu za umma. __16__ takataka __17__ hutapakaa kila mahali ni hatari kwa afya zetu.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 13. A. iliyopita | B. yaliyopita | C. zinazopita | D. zilizopita |
| 14. A. anakaribishwa | B. amekaribishwa | C. alikaribishwa | D. tutamkaribisha |
| 15. A. kujiepusha na | B. kuepushwa na | C. kuebuka na | D. kujiebusha na |
| 16. A. Kicha cha | B. Vifurushi za | C. Mabiwi ya | D. Matita ya |
| 17. A. ambayo | B. ambao | C. ambalo | D. ambacho |

***Kuanzia swali la 18 hadi la 27, jibu swali kulingana na maagizo.***

18. ***Andika wingi wa sentensi:***
Mti ule wa mparachichi ulizaa parachichi tamu. ________________________

19. Nomino, **'marashi na maarifa'** zinapatikana katika ngeli gani?

____________________________________________________

20. ***Tambua aina ya neno lililopigiwa mstari katika sentensi:***
Mwalimu wangu anafundisha lakini <u>wako</u> anasoma gazeti.

____________________________________________________

21. ***Panga maneno yafuatayo kuunda sentensi sahihi:***
kisha nyumbani darasa wanafunzi lao walifagia wakaenda.

____________________________________________________

22. ***Andika sentensi ifuatayo upya kulingana na maagizo:***
Nilimkuta mama nilipopitia mto Kwekwe. Anza kwa: Nilipopitia mto kwekwe

____________________________________________________

23. ***Geuza katika usemi wa taarifa:***
Kocha aliwaambia wachezaji, "Tutaendelea kufanya mazoezi msimu huu"

____________________________________________________

24. Je, shairi lililo na mishororo minne katika kila ubeti huitwaje?

____________________________________________________

25. ***Tambua kitenzi kisaidizi katika sentensi:***
Wanafunzi wangali wanacheza uwanjani. ________________________

26. Sentensi: "Mwalimu akifika tutaanza kusoma" ipo katika hali yakinishi. Iandike upya katika hali kanushi. ________________________

27. Salome hufanya kazi kwa bidii sana. Je, ni istiari gani inayoweza kutumiwa kuelezea tabia ya Salome?

____________________________________________________



CamScanner

**4. Fasihi**

**28. *Soma wimbo ufuatao kisha ujibu maswali:***

Kitoto kivivu aiya aiya
Kikienda skuli aiya aiya
Saa tatu hazijafika aiya aiya
Ndicho hicho chalia njaa aiya aiya
"Ticha naona njaa aiya aiya"
Mwalimu hadiriki kuandika lolote aiya aiya
Kitoto machozi yatoka aiya aiya
Hadi ruhusa kipewe aiya aiya
Kitazame kilocho ndani ya chupa aiya aiya
Ndipo kitulie aiya aiya

a) Wimbo huu ni wa aina gani? (alama 1)

____________________________________________________________

b) Eleza sifa tatu za wimbo wa aina hii (alama 3)

____________________________________________________________

____________________________________________________________

____________________________________________________________

c) Taja wahusika wawili katika wimbo huu. ____________________________ (alama 2)

d) Andika maudhui mawili yanayojitokeza katika wimbo huu. ____________________ (alama 2)

e) Andika umuhimu wa nyimbo za aina hii. ____________________________ (alama 2)

**5. Dondoo**

**29. *Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali.***

Chale alijikokota hadi sebuleni. Aliketi kabla ya yeyote katika aila yake kufika hapo. Alikalia kochi lake la kawaida. Moyo ulimdunda alipomwona baba yake akiingia sebuleni. Kama alivyokuwa ametabiri, macho ya baba yake yalipenya hadi moyoni mwake. Yalimpekua Chale kuanzia utosini hadi wayoni akiwa pale alipokuwa ameketi. Yalipotua kwenye mguu wake wa kulia, yaliganda hapo kama barafu kwenye jokofu. Chale aliuhisi mtazamo wa baba yake lakini hakuinua macho yake kumtazama. Tangu kisa cha siku iliyotangulia kule bwawani, Chale hakuwa na ujasiri wake wa kawaida wa kutangamana na baba yake. Alihisi kwamba yeye ndiye aliyekuwa chanzo cha wale mifugo kuvamia shamba la jirani. Alitarajia kuambiwa kwamba alikuwa amewazuzua wenzake kwa ule ucheshi wake na kuwasahaulisha jukumu lao. Mzee Jibrili aliuona wasiwasi uliokuwa kipajini pa mwanawe. Moyo ulimtuma kumuuliza kiini cha wasiwasi huo lakini alijiambia kwamba wakati wa hayo bado ulikuwepo. Walihitaji kuanza siku kwa dua, si kwa kesi.

a) Eleza masuala mawili yanayojitokeza katika dondoo hili.

____________________________________________________________

b) Taja aina mbili za mandhari zinazojitokeza katika dondoo hili.

____________________________________________________________

c) Eleza sifa tatu za Chale kulingana na dondoo hili.

____________________________________________________________

d) Katika dondoo hili, mwandishi ametumia mbinu za lugha tofauti tofauti kuwasilisha mawazo yake. Eleza mbili kati ya mbinu hizo.

____________________________________________________________



CamScanner

# TARGETER WINGS
# JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT

Wings 004

# GREDI YA SABA - 2024
## SEHEMU B:
## KISWAHILI : INSHA

***MUDA: Dakika 40***

| | |
|---|---|
| **Jina** ______________________________ | |
| **Shule** ______________________________ | |
| **Nambari ya Usajili:** ________________ | **Tarehe** ________________ |

**SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI**

1. Kwenye nafasi zilizoachwa hapo juu **andika jina lako na jina la shule yako.**

2. Sasa fungua karatasi hii, soma kichwa cha insha kwa makini na uandike insha yako kwenye nafasi uliyoachiwa.

**Kijitabu hiki kina kurasa 4 zilizopigwa chapa.**

*© Hutungwa na kuchapishwa na Targeter Educational Publishers Ltd Email:info@targeterpublishers.co.ke*

**FUNGUA KURASA**

CamScanner

***Mweleleze mgeni jinsi ya kufika shuleni kutoka sokoni. Katika insha yako zingatia:***

***i) Njia atakayotumia.***

***ii) Safari itachukua muda upi.***

***iii) Atapitia vituo vipi?***

***iv) Ataona vitu gani njiani ili asipotee.***



CamScanner